

**MAKAO MAKUU**

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole

S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

## TANGAZO KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA BABATI (BABATI WSSA) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

#### Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-017-2018/2019

Mnamo tarehe 12 Novemba 2018 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Babati (Babati WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Majedwali namba 1 hadi 3 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na bei zinazopendekezwa

#### Jedwali Na 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Mabadi liko (%)	Bei Zinazopendekezwa				
	2017/18		2018/19	Mabadi liko (%)	2019/20	Mabadiliko (%)	2020/21
Majumbani							
Daraja 1 (0- m <sup>3</sup> 5)	925	69%	1,563	3%	1,604	5%	1,689
Daraja 2 (6- m <sup>3</sup> 10)	1,085	69%	1,834	3%	1,881	5%	1,982
Daraja 3 (>m <sup>3</sup> 10)	1,195	69%	2,020	3%	2,072	5%	2,183
Taasisi	1,610	69%	2,721	3%	2,791	5%	2,941
Biashara	1,890	69%	3,194	3%	3,277	5%	3,452
Viwanda	1,890	69%	3,194	3%	3,277	5%	3,452
Viwanda vya Vinywaji	-	-	3,514	3%	3,605	5%	3,797
Magati	500	69%	845	3%	867	5%	913

#### Jedwali Na.2: Ada ya Maunganisho ya Huduma ya Maji ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Inayopendekezwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Makundi Yote ya Wateja	Asilimia Ishirini (20%) ya Gharama za Maunganisho kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013	Asilimia Ishirini (20%) ya Gharama za Maunganisho kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013		

**Jedwali Na.3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa huduma)**

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19	Mabadiliko (%)	2019/20	Mabadiliko (%)	2020/21
Majumbani	10,000	50%	15,000	0%	15,000	0%	15,000
Taasisi	10,000	150%	25,000	0%	25,000	0%	25,000
Biashara	10,000	100%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Viwanda	10,000	100%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Viwanda vya Vinywaji			20,000	0%	20,000	0%	20,000
Magati	10,000	50%	15,000	0%	15,000	0%	15,000

Kwa Mujibu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati, sababu kuu ya kuomba marekebisho ya bei za huduma zake ni kushindwa kumudu ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo kutokana na bei zisidhokidhi hali halisi ya gharama za huduma, kuanzishwa kwa tozo mbalimbali (kama vile Kodi ya Uendelezaji Ufundi Stadi na Kodi ya Ongezeko la Thamani katika vifaa) na kuondolewa kwa tozo ya huduma.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumatano, tarehe 6 Februari 2019 katika Hoteli ya White Rose** iliyopo Babati Mjini kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Mamlaka ya Maji Babati, na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 11 Februari 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA KASKAZINI, GHOROFA YA PILI, JENGO LA PPF; JIRANI NA HOTELI YA KIBO PALACE, ARUSHA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BABATI**.

**Imetolewa na:**  
**Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**  
**(EWURA)**

**2 Januari 2019**